Jarida la kila wiki la Halmashauri

# Nsimbo Wiki hii

Tunatekeleza .......

www.nsimbodc.go.tz

TOLEO NA.07

MACHI 16 ,2019

## Ujenzi,Ukarabati Kituo cha Afya Katumba Nsimbo mbioni kukamilika,

- *Kuwekewa Jiwe la Msingi na Mwenge wa Uhuru Aprili,2019*
- *Injinia wa Ujenzi Nsimbo Ufuatiliaji Masaa 24,*
- *Wananchi punde kufaidi matunda ya Utekelezaji Ilani,*



















***Pichani:****Hali ya Utekelezaji ya Ujenzi na Ukarabati katika Kituo cha Afya Katumba Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo hadi kufikia Machi 7,2019.Picha Na.1.Lango la kuingilia Kituo cha Afya Katumba,Picha Na.2,Nyumba ya Mganga,Picha Na.3,Jengo la Maabara,Picha Na.4,Wodi ya akina mama na Jengo la Upasuaji,Picha Na.5,Jengo la Kuhifadhia Maiti,Picha Na.6,Jengo la X-Ray.*

# Ujenzi Ukarabati Kituo cha Afya Katumba mbioni kukamilika

**Na: John Mganga,**

*Nsimbo-Katumba,*

Ujenzi na Ukarabati unaoendelea katika Kituo cha Afya Katumba Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ikiwa ni maboresho ya Kituo hicho cha Afya kikongwe Nsimbo uko katika hatua nzuri na ya kuridhisha ***Nsimbo wiki hii*** linatanabaisha

Injinia wa Ujenzi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Golden Katoto** Machi 8, 2019 alitembelea kituo hicho cha Afya ikiwa ni utekelezaji wa ratiba aliyojiwekea kutembelea mara kwa mara kufuatilia kwa karibu hatua ya Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho unaotekelezwa chini ya Mafundi Wazawa(Local Fundi).

Akizungumzia hali ya Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho Injinia Katoto amesema hatua ya Ujenzi Kituoni hapo ni ya kuridhisha kutokana na jitihada na hatua ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imekuwa ikizichukua ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Ujenzi huo unasimamiwa kwa karibu muda wote lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa hakuna kitu kinaharibika kwa kuwa tayari Mafundi hao wamekwisha lipwa kwa kazi ambazo zimekwisha fanyika.

Akiwa katika ukaguzi Kituoni hapo **Injinia Katoto** amewaelekeza wasimamizi wa Mafundi wengine kuhakikisha kuwa wanazingatia muda wa kukamilika kwa Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho kama ilivyo katika Mkataba.

Amewashauri mafundi wakuu kuhakikisha kuwa wanawalipa stahiki zote za Wafanyakazi na Vibarua wanaofanya nao kazi kwa wakati ili kuondoa mazingira yanayoweza kuchochea Vibarua na Wafanyakazi hao kukosa uaminifu na kujihusisha na vitendo vya wizi wa Malighafi za Ujenzi Kituoni hapo jambo linaloweza kuathiri kukamilika kwa wakati kwa mradi huo.



*Pichani:Injinia wa Ujenzi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Golden Katoto(Aiyesimama Kulia ) akiwasikiliza baadhi ya Vibarua na Wafanyakazi wanaofanya kazi ya Ujenzi na Ukarabati katika Kituo cha Afya Katumba alipofanya ukaguzi Kituoni hapo Machi 8,2019.*

Injinia Katoto amefafanua kuwa kitendo cha baadhi ya Wasimamizi katika maeneo kadhaa wamekuwa wakiathiri kazi zao na wakati mwingine kupoteza uaminifu kwa Taasisi wanazofanya nazo kazi kutokana na kuchelewesha malipo kwa Wafanyakazi na vibarua katika maeneo yao ya kazi jambo linalopelekea kutokamilika kwa wakati kwa kazi.

Kituo cha Afya Katumba ni moja kati ya Vituo vya Afya Nchini vilivyopewa na Serikali Jumla ya Mil.600 kwa ajili ya Ujenzi na Ukarabati ili kuboresha utoaji wa huduma za Afya kwa kiwango kinachoridhisha kwa Wananchi

Ujenzi unaondelea katika Kituo hicho ni pamoja na Ujenzi wa wodi ya Wazazi pamoja na Chumba cha Upasuaji ,Ujenzi wa Nyumba ya kisasa ya Mganga wa Kituo hicho,Maabara,chumba cha Kuhifadhia maiti pamoja na Jengo la Mionzi(X-Ray)ambapo kwa mujibu wa Mratibu wa Mwenge wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo mradi huo unatarajiwa kuwekewa Jiwe la Msingi Aprili,2019 katika Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

# Wataalamu wa Afya Nsimbo watakiwa kuelekeza Elimu ya Afya Kijijini

**Na: John Mganga,**

*Nsimbo-Makao Makuu,*



*Pichani :Mwenekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mh.Raphael Kalinga akizungumza wakati wa Semina ya siku moja kujenga Uelewa kwa Watumishi juu ya Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele iliyofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri Machi 14,2019.Kulshoto ni Kaimu Mkurugenzi siku hiyo Bw.James Kombo na Kushoto ni mratibu wa Magonjwa yasiyopewa kipaumbele NsimboBi Marrystellah Mdogo.*

Wataalamu wa Idara Ya Afya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wametakiwa kuandaa mikakati madhubuti itakayowezesha Jamii kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu za kudhibiti na kujikinga na Magonjwa yasiyopewa kiaumbele na Jamii.

Mratibu wa Magonjwa yasiyopewa kipaumbele Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bi.Merrystellah Mdogo, katika Semina ya siku moja ya kujenga uelewa kuhusu Magonjwa hayo iliyofanyika Machi 14, 2019 katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri,ameeleza kuwa Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele na Jamii ni Magonjwa ambayo yamo ndani ya Jamii masikini lakini viongozi na hata Jamii yenyewe hawayapi kipaumbele.

Bi Marrystellah Ameyataja Magonjwa hayo kuwa ni Usubi unaosababishwa na Minyoo ienezwayo na Inzi Weusi wanaokaa kandokando ya mito iendayo kasi, unaosababisha ngozi kuwasha na kuwa na mabakamabaka,Matende na Mabusha unaosababishwa na minyoo inayosambazwa na mbu aina ya Qulex unaopelekea miguu,matiti na korodan za Mwanaume kuvimba,Kichocho kinachosababishwa na Minyoo inayoenezwa na Konokono,Trakoma, isababishwayo na Bakteria, wanaosambazwa na Inzi, pamoja na Minyoo ya Tumbo

Akifungua Mafunzo hayo ya siku Moja Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mh.Raphael Kalinga amewataka wataalamu hao wa Idara ya Afya Nsimbo kuhakikisha kuwa Jamii inakuwa na Uelewa na inayapa uzito Magonjwa hayo ili kudhibiti madhara yatokanayo na magonjwa hayo.

Kalinga ameeleza kuwa Uelewa mdogo kwa Jamii kuhusu Magonjwa yatokanayo na Minyoo a na Bakteria imekuwa sababu kubwa ya kuenea kwa magonjwa hayo katika maeneo mengi hali inayopelekea magonjwa hayo kukomaa na kusababisha madhara kwa Jamii.

Kufuatia hali hiyo Mwenyekiti Kalinga ametoa wito kwa wataalamu wa Afya Nsimbo pamoja na mikakati madhubuti ya kufikisha elimu kwa Jamii amewataka pia kuhakikisha kuwa elimu ya matumizi sahihi ya dawa za kujikinga inatolewa ipasavyo Mashuleni kwa kushirikiana kwa karibu na walimu ili kupunguza tatizo hilo.

Katika Semina hiyo washiriki wa mafunzo hayo walifanya mdahalo kuhusu magonjwa yasiyopewa kipaumbele ambapo baadhi ya washiriki walipata fursa ya elimu juu ya mitazamo hasi waliyokuwa nayo juu ya njia zinazoeneza baadhi ya magonjwa ikiwemo Matende na Mabusha.

Kupitia Mdahalo huo Mratibu wa Magonjwa yasiopewa kipaumbele Nsimbo Bi.Marrystellah Mdogo alitoa elimu ya namna ya kujikinga na Magonjwa hayo yatokanayo na Minyoo na Bakteria,pamoja na umuhimu wa kujikinga na magonjwa hayo.

# Kalamu ya Mhariri



## Amani,Upendo mahala pa kazi ni chachu ya utoaji huduma bora kwa Wananchi.

*Ndugu zangu,*

*Nitumie fursa hii kuwapongeza Watumishi wa kada zote wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa namna ambavyo mmekuwa mkiwajibika katika Vituo vyenu vya kazi katika kuhakikisha kuwa Wananchi wanapata huduma bora kwa kiwango kinachoridhisha,kipekee kwa Moyo wenu wa kujitoa na wenye dhamira ya dhati ya kuwaletea Wanansimbo Maendeleo.*

*Katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya Utoaji huduma kwa Wananchi kama Watumishi wa Umma yapo mambo ya Msingi ambayo tunapaswa kuyazingatia ili kuboresha Mazingira ya kazi na hivyo kuimarisha utoaji huduma.*

*Miongoni mwa mambo hayo ni Amani na Upendo mahala pa kazi.Kama Watumishi wa Umma tunalo jukuu kubwa sana la kuhakikisha kuwa tunadumisha Amani ,Upendo na utulivu mahala pa kazi .*

*Amani ni kila kitu asikuambie mtu,Palipo na amani hakuna jambo linakwama,palipo na amani yapo maridhiano,palipo na Amani pana Upendo, palipo na upendo pana Mungu na Palipo na Mungu hakuna Jambo linaloshindikana.*

*Wakati tukijizatiti na kufunga mikanda katika kuhakikisha kuwa Mwananchi wa Nsimbo anapata huduma bora na za kuridhisha ni muhimu pia kuhakikisha kuwa kila mmoja wetu anabeba jukumu kubwa la kudumisha Amani ,Upendo na Utulivu ili kuboresha mazingira ya kazi na hivyo kuboresha utoaji huduma bora kwa Wananchi.*

*Watumishi wa Umma wakiwa kitu kimoja ,wakapendana wenyewe kwa wenyewe,wakavumiliana na kusameheana katika mambo kadha wa kadha ni rahisi sasa Upendo huo kutoka Nje na Mwananchi akahudumiwa kwa tabasamu.*

*Tudumishe Amani na Utulivu mahala pa kazi,tuimarishe huduma bora kwa Wananchi.*

*jhndoctor@gmail.com*

*Tel-0746310716*

# MATUKIO KATIKA PICHA

*Pichani :Mratibu wa NTDS ,Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bi.Marrystellah Mdogo akichokoza Mjadala unaohusu Imani potofu zilizoenea katika jamii kuhusu njia ya kuenea kwa Baadhi ya Magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Jamii ikiwemo Matende na Mabusha.*



*Pichani: Injinia wa Ujenzi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Golden Katoto(Mwenye Shati Jekundu)akifafanua Jambo mbele ya Diwani wa Kata ya Katumba Mh.Seneta Baraka Jeti(Mwenye T.Shirt Nyeusi)na maadhi ya Wtaalamu wa Kituo hicho cha Afya Katumba Machi 4,2019 katika Ziara ya Ukaguzi wa Ujenzi na Ukarabati Kituoni hapo*



*Pichani: Baadhi ya Watumishi washiriki wa Semina ya siku Moja ya NTDS wakiwa katika Mjadala kuhusu Imani potofu zilizojengeka katika Jamii kuhusu njia za kuenea kwa baadhi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele na Jamii ikiwemo Matende na Mabusha*



Jarida hili la Wiki Nsimbo huandaliwa na kutolewa na Kitengo cha Teknolojia ya Habari Mawasiliano na Uhusiano Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ,Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo,Ofisi Na.2


**Mawasiliano:**

**Mkurugenzi Mtendaji,**

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

SLP 688,Mpanda Katavi

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz

Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

Tel +25546310716